

MAOMBI YA REHEMA

Mungu, wewe ni wa rehema, na ni mwingi wa fadhili kwa watu wote wakuitao (Zaburi 86:5). Lakini Wewe, Bwana, U Mungu wa rehema na neema, Mvumilivu, mwingi wa fadhili na kweli (Zaburi 86:15).

Bwana umejaa huruma na neema, Huoni hasira upesi, ni mwingi wa fadhili (Zaburi 103:8). Nami nimezitumainia fadhili zako; Moyo wangu na uufurahie wokovu wako (Zaburi 13:5). Bwana, dhihirisha fadhili zako za ajabu Wewe uwaokoaye wanaokukimbilia; Kwa mkono wako wa kuume Uwaokoe nao wanaowaondokea (Zaburi 17:7). Maana fadhili zako ni njema kuliko uhai; Midomo yangu itakusifu (Zaburi 63:3). Wewe ni mwenye upendo, neema, fadhili, na rehema zimejaa na wewe tu hapana mwingine.

Rehema nyingi zipo na wewe, Ee Mungu uliyeketi mahali pa juu palipo inuka, kwenye kiti kilicho na utukufu, kiti kilicho na nguvu, kiti kilichofunikwa na upendo wako, kiti kilichofunikwa na wingu lako la neema, kiti kilichofunikwa na nguvu na uweza. Ni kiti kilichozungukwa na malaika, ni kiti kilichozungukwa na wazee ishirini nne na wenye uhai wa nne. Hakika hiki ni kiti chenye nguvu kilicho juu sana kupita mbingu zote. — CONNECT —

Ee Mungu ninakiri kwamba wewe ni Mungu uliyeumba mbingu na nchi, na vyote vilivyomo ndani yake, vilivyoko juu mbinguni, angani, katika nchi, chini ya nchi, vyote uliumba wewe. Ninakiri wewe ni Mungu mwenye nguvu sana.

Rehema zako ziwe kwangu, neema yako iwe kwangu, upendo wako uwe kwangu, Unirehemu, Bwana , mwana wa Daudi! Unirehemu, unirehemu, unirehemu, Bwana, mwana wa Daudi (Mathayo 20:30). Ee Mungu wangu uni rehemu. Nahitaji rehema zako. Nahitaji upendo wako unifunike , mimi ni muovu. Nimechafuliwa na dhambi, nimekukosa wewe , dhambi imeniharibu, dhambi imenitenga na wewe, ni rehemu sasa.

Uso wako usiondoke kwangu, ulinzi wako usiondoke kwangu, nahitaji ulinzi wako, mafuta yako yasiondoke kwangu, wala Roho wako Mtakatifu asiondoke kwangu (Zaburi 51:11), mkono wako usiondoke kwangu, unikumbatie kwa huruma yako. Usinifiche siri zako. Na uwepo wako uwe kwangu.

Mungu, wewe ni mvumilivu, sijawahi ona Mungu mvumilivu kama wewe, ulisema katika Luka 18:7 " Na Mungu, je! hatawapatia haki wateule wake wanaomlilia mchana na usiku naye ni mvumilivu kwao? ", sisi wanadamu tunakosea, tunakutenda dhambi, tunakuudhi, unasema nasisi lakini tunakataa kusikiliza sauti yako, tunatembea nje ya njia zako, lakini wewe ni mwaminifu, na mvumilivu siku zote, bado unatupa nafasi nyingine ya kutubu na kurudi kwako kama mwanampotevu alivyorudi kwa baba yake, huu ni upendo wa ajabu sana kwetu.

Unatuhifadhi, unatulinda, unatulisha, unatuvisha. Hakika toka nitoke tumboni mwa mama yangu, sijawahi ona Mungu kama wewe, Mungu mwenye kusamehe, mvumilivu.

Tunapokuwa mbali nawe, bado unatuita tuwe karibu nawewe, tunapotenda dhambi bado unarehemu, Wewe ulisema dhambi zako ziwapo nyekundu kama damu, zitakuwa nyeupe kuliko theluji, tena hutazikumbuka kabisa.

Bado unatuita unasema njooni kwangu ninyi nyote wenye kulemewa na mizigo ya dhambi nami nitawapumzisha, ukasema jitieni nira yangu, mjifunze kwangu; kwa kuwa mimi ni mpole na mnyenyekevu wa moyo; nanyi mtapata raha nafsini mwenu kwa maana nira yangu ni laini, na mzigo wangu ni mwepesi, Yesu natua mizigo yangu dhambi kwako, ziwe za kwangu binafsi, familia yangu, ukoo wangu, ndugu zangu, kabila langu, nchi yangu.

Ee Mungu, unajua upumbavu wangu, Wala hukufichwa dhambi yangu (Zaburi 69:5). Tumetenda dhambi pamoja na baba zetu, Tumetenda maovu, tumefanya ubaya (Zaburi 106:6). Maana dhambi zangu zimenifunikiza kichwa, Kama mzigo mzito zimenilemea mno (Zaburi 38:4). Kwa maana nitaungama uovu wangu, Na kusikitika kwa dhambi zangu (Zaburi 38:18). Nami nasema, Bwana, unifadhili, Uniponye roho yangu maana nimekutenda dhambi (Zaburi 41:4).

Unioshe kabisa na uovu wangu, Unitakase dhambi zangu (Zaburi 51:2). Maana nimejua mimi makosa yangu Na dhambi yangu i mbele yangu daima (Zaburi 51:3). Usitiri uso wako usitazame dhambi zangu; Uzifute hatia zangu zote (Zaburi 51:9). Kama mashariki ilivyo mbali na magharibi, Ndivyo ulivyoweka dhambi zetu mbali nasi (Zaburi 103:12). Bwana neno lako nalikae ndani yangu nisije nikakutenda dhambi (Zaburi 119:11).

Yesu, wewe hukuja kuwaita wenye haki bali wenye dhambi (Mathayo 9:13). Bwana, usikumbuke tena uovu wangu. Osha nafsi yangu, roho yangu na mwili wangu kwa damu yako takatifu. Safisha akili yangu, mawazo yangu, kumbukumbu zangu safisha kwa damu yako Yesu wangu. Ondoa mawazo machafu, kumbukumbu chafu katika akili yangu. Ondoa sauti za kipepo, mizimu, kishetani, katika masikio yangu, akili yangu, moyo wangu, na nafsi yangu kwa damu yako takatifu. Futa picha chafu ambazo ibilisi ameweka ndani ya akili yangu, mawazo yangu, kumbukumbu zangu.

Yesu niondolee kutokusamehe kwangu, kwa maana umesema tukiwasamehe watu makosa yao, na Baba yetu wa mbinguni atatusamehe sisi makosa yetu (mathayo 6:14). Yesu, nipe moyo wa kusamehe. Naomba moyo ulipondeka wenye huruma, uvumilivu, na wenye hofu yako.

Napokea msamaha wako Yesu, nasema asante kwa msamaha wa dhambi zangu. Nifunike kwa damu yako, uwepo wako, ulinzi wako uwe kwangu. Nijaze Roho wako Mtakatifu maradafu, nipake mafuta ya Roho Mtakatifu juu yangu. Huisha kila kilicho kuwa kimekufa ndani yangu, rudisha kila kitu ambacho kilikuwa kimeibiwa na Ibilisi ndani yangu au nje yangu. Kwasababu neno lako linasema katika mithali 6:30-31 “Watu hawamdharau mwivi, akiiba ili kujishibisha, iwapo aona njaa; Lakini akipatikana atalipa mara saba; atatoa mali yote ya nyumba yake.” Asante Yesu wangu katika jina la Yesu. Amina!

By Innocent Morris

+255766259750

Instagram Page: **holyspiritconnect**